

MLINZI, HABARI GANI ZA USIKU?



[Ndugu Gene Goad anasoma Isaya 21:1-12—Mh.]

[Mzigo juu ya jangwa la bahari. Kama vile tufani za kusini zipitavyo; ndivyo inakuja kutoka jangwani, kutoka nchi ya kutisha.]

[Nimetangaziwa maono ya kusikitisha; atendaye hila anatenda hila, mharibifu anaharibu. Panda juu, Ee Elamu: husuru, Ee Umedi; mimi ninakomesha maombolezo yake yote.]

[Kwa sababu hiyo viuno vyangu vimejaa maumivu, utungu umenishika, kama utungu wa mwanamke azaae: naliuwa sana niliposikia; Nilifadhaika kwa hofu kuiona.]

[Moyo wangu ulidunda, woga ukanitia hofu: giza-giza la jioni nilipendalo limegeuka likanitetemesha.]

[Tayarisha meza, weka ulinzi katika mnara: kula, kunyweni: inukeni, enyi wakuu, tieni ngao mafuta.]

[Maana Bwana aniambia hivi, Enenda, weka mlinzi, aonayo na ayatangaze.]

[Naye akaona gari pamoja na baadhi ya wapanda farasi, gari la punda, na gari la ngamia; naye akajitahidi kasikiliza kwa makini sana:]

[Ndipo akalia, Simba: Bwana wangu, mimi husimama daima juu ya mnara wakati wa mchana, na kila usiku ninakaa zamu ya ulinzi wangu:]

[Na, tazama, linakuja gari lililokaa watu, pamoja na baadhi ya wapanda farasi. Akajibu, akasema, Babeli umeanguka, umeanguka; na sanamu zote za kuchonga za miungu yake amezivunja chini.]

[Ee kupura kwangu, na nafaka ya sakafu yangu: hayo niliyoyasikia kwa BWANA wa majeshi, Mungu wa Israeli, nimewapasha habari zake.]

[Mzigo wa Duma. Ananililia kutoka Seiri, Ee Mlinzi, habari gani za usiku? Ee Mlinzi, habari gani za usiku?]

[Mlinzi akasema, Asubuhi inakuja, na usiku pia: mkitaka kuuliza, ulizeni: rudini, njoni.]

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

² Asante, Ndugu Neville. Ni vizuri kukuona tena.

³ Habari za asubuhi, kwa darasa letu la Biblia asubuhi ya leo, kwa kuwa tunapenda kuwasalimu katika Jina la Bwana Yesu. Nilipokuwa nikiendesha motokaa barabarani muda mfupi tu

uliopita, pamoja na familia yangu, nilikuwa nikiwazia juu ya watu wanaotoka kuja kanisani siku za utelezi kama hizi, wakati theluji imejaa kote nchini, hatari sana barabarani. Hawaji wapate kuonekana tu. Wana kusudi fulani la kuja. Nami nina furaha sana kuona kundi hili hapa asubuhi ya leo, ambalo, bado, “Imani ya baba zetu, ingali inaishi,” inawaka katika mioyo ya wanaume na wanawake kila mahali.

⁴ Neno limesomwa hivi punde na Ndugu yetu Gene Goad, kwenye sura ya 21 ya Kitabu cha Isaya, ambapo tutasomea, kwa muda, na kisha tufanye maombi kwa ajili ya wagonjwa. Na sasa kwa ajili ya somo, asubuhi ya leo, ningetaka kuchukua kutoka hapo, kifungu cha 11 hadi cha 12: *Mlinzi, Habari Gani Za Usiku?*

⁵ Na kabla hatujaanza kunena, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo katika maombi.

⁶ Bwana Mungu, Wewe ndiwe Mungu wa baba zetu. Wewe ndiwe Mungu uliyepulizia pumzi ya kwanza ya uhai iliyopata kuja duniani, na umekuwa na udhibiti wa kila uhai hadi wakati huu wa sasa, na utadhibiti milele. Kwa maana Wewe ndiwe Muumba wa wanadamu wote, na vitu vyote vinavyopumua. Wewe ndiwe Muumba.

⁷ Nasi tuna furaha, asubuhi ya leo, kuamini mioyoni mwetu ya kwamba ahadi Zako ni za kweli, kila moja yao. Na ya kwamba katika ahadi hizi, umesema ya kwamba popote wawili watatu walipokusanyika katika Jina Lako, ya kwamba ungekuwa katikati ya watu Wako, na kwamba utaitikia wito wao.

⁸ Na kuna mioyo mizito leo. Kwa kuwa tangu niingie humu kanisani, ninawaona wale walio kwenye machela au vitanda vya wagonjwa. Na wengine wamekunja mikono ya nguo zao, kutokana na maambukizi—maambukizi mikononi mwao. Na wengine, nimesikia, ambao wamewapoteza wapendwa. Na, loo, ni ulimwengu wenye dhambi na mwovu! Lakini, hata hivyo, mambo haya yote hayana budi kuthibitika katika Bwana Yesu, Yule aliyetwambia, kwamba, “Mambo yote yanafanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu.”

⁹ Nasi tumefarijiwa asubuhi ya leo, kuamini kwamba mengi ya mambo haya ni ya kututiisha. Nasi tunapenda kuwazia juu ya Maandiko, kwamba, “Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya. Watapaa juu kwa mabawa kama tai. Watakimbia wala hawatachoka. Watatembea wala hawatazimia.” Na kama mshairi alivyosema, “Nifundishe, Bwana. Nifundishe, Bwana, jinsi ya kungoja.”

¹⁰ Tujalie, leo, tunapongojea kusikia kutoka Utukufuni, na kutoka kwa kinywa cha Mwokozi wetu, kupitia kwa Roho Mtakatifu, kwamba tutangojea kwa saburi kusikia Sauti Yake ikitunenea mambo ya kutupendeza, kupitia Neno Lake, na kunena msamaha wa dhambi zetu, na uponyaji wa magonjwa yetu.

¹¹ Na jalia tuondoke kwenye maskani hii asubuhi ya leo, tukishangilia, na kusema kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa maana tunaamini kweli kwamba Yeye ni Bwana aliyefufuka, kama walivyomwona siku hiyo. Naye yuko miongoni mwa watu. Hatutachoka, mioyo yetu haitazimia. Jalia tu tufanye upya imani yetu, kila saa, ndani Yako. Tujalie, Baba.

¹² Tunakuomba ulibariki Neno lililoandikwa. Na kubariki masikio yatakayosikia, na midomo itakayonena; na ukipatie Mwenyewe Utukufu. Maana katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

¹³ Hakuna mmoja wetu ambaye hawezi kupatwa na matatizo. Mungu hajaahidi kutuepusha na magonjwa yote. Lakini imeandikwa, kwamba, “Nguvu Zake zinatoshia, na Yeye kamwe hataweka mengi sana juu yetu ila yale atakayotupa neema ya kustahimili.” Kwa hivyo tunayo hiyo faraja ya kujua.

¹⁴ Tuelekee kwenye wazo la somo sasa hivi, kwa dakika chache, juu ya jambo lililoonekana kuwekwa moyoni mwangu saa chache zilizopita: *Mlinzi, Habari Gani Za Usiku?*

¹⁵ Labda ilikuwa yapata, kati ya machweo ya jua na kuingia giza. Na ingekuwa ni siku ya kuogofya humo mjini, kwa kuwa onyo lilikuwa limetolewa, ambalo wao, yule mlinzi kwenye mnara, alikuwa amewahadharisha kwamba aliona kwa mbali mavumbi yakipanda kutoka kwenye magurudumu ya magari ya farasi. Naye akasikia vishindo vya kwato za farasi, kwa mbali sana.

¹⁶ Lakini kama vile wasichana wawili wangekuwa wamesimama kisimani, na katika umri wao mdogo, wa ujana, walikuwa na mengi zaidi ya kuwazia, walifikiri, kuliko kile neno la mlinzi huyu lilichokuwa. Labda halikumaanisha mengi sana kwao, kwa sababu walikuwa tu katika upeo wa ujanajike. Labda ilikuwa ni kwa sababu kulikuwa na karamu usiku huo, nao wasichana hawa walitaka kuhudhuria karamu hii. Na ilionekana kana kwamba onyo la huyo mlinzi lisingekuwa na athari juu ya yale waliyokuwa wamekusudia anasa zao za dunia usiku huo. Kwa hivyo vile mazungumzo yangeendelea, na—na msichana mmoja angemwambia huyo mwingine, “Je, si ni vibaya sana, kwamba, katika siku zetu, kwamba tuna waondoa-furaha kama hao, mtu ambaye angejaribu ku—kutuondoa katika majaliwa tuliyo nayo, na kutoka katika starehe ambazo tungeweza kufurahia?”

¹⁷ Nami ninaamini hiyo ingeendana na mtindo wa kisasa wa siku hizi, ambapo watu wanajaribu kuwazia kwamba unapojaribu kuwa macho na kuwaonya juu ya hatari zinazokaribia, kwamba wanaonekana kufikiri kwamba wewe ni mzee tu asiyelewa, mtu ambaye anajaribu kuondoa furaha yote maishani.

¹⁸ Nasi tungewazia tena juu ya vijana, walipokuwa wakitoka kwenye karakana, nazo nyuso zao ni chafu kutokana na kazi waliyokuwa wakifanya mchana. Basi kijana mmoja anaweza kumwambia mwenzake, “Mara tutakapooga na kujiandaa, kidogo, mbona, tutakutana kwenye kilabu ya pombe, kama kawaida. Kwa maana nina hakika kwamba wewe, John, hujafadhaishwa na habari ile tuliyoisikia leo, yule mlinzi kwenye mnara, akijaribu kuondoa furaha yote maishani, akijaribu kutwambia kwamba kuna hatari inayokaribia. Lakini, mnajua, tuna jeshi bora zaidi lililopo. Na wengi wa askari wetu huninii. . . hukutana kila usiku mahali hapa tunapokutana sisi, nasi tunafurahia ushirika wa pamoja, kama vile ku—kucheza kidogo kamari ya kirafiki, na vinywaji vichache. Nami, kwangu mimi,” angesema, “nakataa kabisa kushtuliwa na upuuzi wowote huu ambao mlinzi huyu angezungumzia. Kwa kuwa tunaamini kama kungekuwako na hatari yoyote inayokaribia, kwamba hakika ma—marabi wetu wangejua habari zake, wachungaji wetu, nao wangekuwa wakitwambia kuhusu mambo kama hayo. Nasi kamwe hatutaki kusikia hadithi hizi za kuchosha za walinzi hawa kwenye mnara.”

¹⁹ Na kama hiyo siyo taswira nzuri ya taifa letu siku hizi, kwamba vijana wa nchi yetu, wala sio vijana tu, bali watu wazima wa nchi yetu, wamerukwa na akili kabisa. Nao wanakataa kusikia maonyo. Na mara tu mlinzi wa kweli anapotoa onyo, anahesabiwa kuwa mzushi, ama mlokole fulani.

²⁰ Na mchana unapozidi kuwa usiku, labda askari langoni, anayeyalinda malango, kidogo anashikwa na wasiwasi. Naye anamwendea nanii. . . mshika doria jirani yake, na kusema, “Je, unaamini kwamba kungekuwako na uwezekano kwamba mlinzi huyo alikuwa anasema kweli?”

²¹ Mnajua, kuna kitu fulani kuhusu hatari, kuna kitu fulani kuhusu kifo, ambacho kinaonekana kuwa na maonyo ya awali. Mara nyingi wapendwa kabla tu ya kuvuka ng’ambo ya pili, inaonekana kuna onyo linalowajia.

²² Ninaweza kukumbuka juu ya baba yangu, kabla hajatuacha. Alikuwa amehama Kentucky kwa miaka mingi. Lakini, kwa ghafla, kitu fulani kilionekana kumjilia baba, ashuke kwenye makazi ya kale na kuzungumza na wapendwa wake na marafiki zake.

²³ Baada ya kurudi nyumbani, ndugu yake, ambaye hakuweza kumwona, alikuwa ameonywa kwa njia ya ajabu kuja Jeffersonville kumwona. Na wakati walipokuwa wameketi, wakizungumza, baba akavuka akaingia ule ulimwengu mwingine.

²⁴ Ninamkumbuka baba mkwe wangu. Siku chache tu kabla ya kuondoka kwake, alisema, “Billy, hebu mimi na wewe twende kuwinda kuchakulo, juu ya Utica. Ninataka tu kwenda

pale mahali pa kale.” Kwa namna fulani, kwa mapenzi ya Mungu, sikuweza kwenda naye siku hiyo. Naye akapanda siku hiyo na kuwinda, na aliposhuka akarudi kwa basi, a—aliniambia, akasema, “Nilikuwa nimeketi juu sana kilimani. Yote yamebadilika sasa. Lakini huko chini kabisa kwenye kona fulani ya msitu, kule Battle Creek, juu yetu tu,” akasema, “ilionekana kana kwamba ningeweza kusikia mama yangu akiita, ‘Loo, Frankie!’” Usiku huo alitoa ushuhuda, katika safu ya pili ya kanisa hili, upande wangu wa kushoto, akiwataka watu wamwombee. Ndipo siku chache baadaye, tukamzika.

²⁵ Inaonekana tu kwamba Mungu daima hutuma mjumbe. Ni wema Wake na neema Yake, kuwapa waaminifu moyoni onyo la mambo yanayokaribia.

²⁶ Nami nina furaha sana kwamba katika siku hii tunayoishi sasa, kwamba, wakati huzuni na giza viko kila mahali, inaonekana kuna tumaini lenye baraka linaloishika mioyo ya watu wa Mungu, kwamba saa fulani tukufu Yesu atakuja.

²⁷ Na katika wakati huu mkuu wa taabu, katika mji huu, vijana wakipuuzwa, na watu wengi ambao hawakujali kuhusu kile mlinzi alisema. Bila shaka, walikuwa kwenye kilabu ya pombe, wakinywa, na karamu ilikuwa ikiendelea. Na askari wote walikuwa wakinywa. Nao walikuwa na wakati mzuri sana, walifikiri walikuwa salama tu walivyoweza kuwa. “Hakuna kitu kitakachowadhuru,” kwa sababu walikuwa tu wamechangamka, tuseme kwa pombe kali za wiski na mchanganyiko wa vinywaji.

²⁸ Na mara ghafula, kukaja magari ya farasi yakifingirika moja kwa moja kuingia mjini. Ndipo milango ya vilabu vya pombe ikavunjwa, na makazi, nazo silaha za kufisha zilikuwa zikifanya kazi, kwa sababu tu walikataa kusikia onyo la yule mlinzi.

²⁹ Na kazi za mlinzi, katika Biblia ya kale, zilikuwa ni mtu aliyechaguliwa. Hana budi kuwa mtu ambaye anazifahamu sayari za mbinguni. Hana budi kujua hasa mahali ambapo nyota zinaning’inia, kuwaambia watu wakati kamili. Wengi wa waliochoka, wangetoka, labda, na hawakuweza kulala, walihangaika, nao wangempigia makelele mlinzi kwenye mnara, nao wangepiga kelele kwa maneno haya, “Mlinzi, habari gani za usiku?”

³⁰ Naye angezitazama nyota, halafu angesema, “Ni wakati *fulani-fulani*.”

³¹ Ndipo wangerudi kitandani mwao, au popote walipochagua kukaa, walingojea kupambazuke, wakati usiku wa kuchosha, usiotulia, wenye wasiwasi, ungekwisha.

³² Mungu aturehemu! Sijui kama si wakati, leo, ambapo hatukumwita Mlinzi wetu mkuu, “Habari gani za usiku?” Kuna hatari inayokaribia, na ulimwengu wote unaonekana kutetemeka chini ya ushawishi wake.

³³ Mlinzi pia ilibidi awe kwenye zamu, nyakati zote. Naye alipaswa kuwaonya watu juu ya hatari zinazokaribia. Huo ulikuwa ndio wajibu wake, kuangalia hatari inayokaribia. Naye alikuwa juu ya mnara uliojengwa juu sana kuliko kuta. Na kwenye mnara huu huko juu, ndani yake, alikuwa na vitabu vya elimu ya nyota, na kadhalika, ili aweze kuzianguka nyota na kujua wakati. Kitu chochote kinachokaribia, wakati wa mchana, angeweza kujua.

³⁴ Kisha, yeye pia angeweza kuona mbali sana kuliko mtu yeyote aliyekuwa chini ardhini. Aliweza kuona mbali kuliko mtu yeyote ukutani, kwa sababu alikuwa huko juu zaidi. Na kadiri unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyoweza kuona mbali. Nawe unaweza kujua hatari zinazokaribia, mbali sana kuliko wale wasioweza kuondoka ardhini.

³⁵ Na kama vile Isaya, katika siku zake, alivyokuwa akinena ya kwamba Mungu alikuwa amemfanya mlinzi. Mungu aliwafananisha manabii wake na tai.

³⁶ Na kama vile nimehubiri mara nyingi juu ya somo la tai, tai ni ndege ambaye anaweza kwenda juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Naye hana budi kuundwa maalum kwa ajili ya mwinuko huo anaolingia. Sasa, mwewe hangeweza kamwe kumfuata. Hakuna ndege mwingine angeweza kumfuata. Yeye ni ndege aliyebwa na Mungu, naye aliambwa hivyo. Ikiwa ndege mwingine angejaribu kuchukua mahali pake, angeangamia. Anapaswa kuwa na manyoya magumu, mbawa zenye nguvu. Basi ingemfaa nini kupaa juu endapo asingeweza kuona, hana macho mazuri ya kuona? Mwewe angekuwa kipofu huko juu; hangeweza kuona. Lakini kadiri tai anavyopanda juu, ndivyo anavyoweza kuona mbali zaidi.

³⁷ Naye Mungu aliwafananisha manabii wake na tai. Hao ndio walinzi wanaopanda juu zaidi, ili waweze kuona mbali zaidi. Nayo macho yao yalifanywa ya kiroho wapate kuona hatari zinazokaribia.

³⁸ Naye Mungu alikuwa amemweka Isaya apate kuwaonya watu kwamba kuna hatari inayokaribia, wala wasingemsikiliza.

³⁹ Na, leo hii, Mungu angali ana tai, ama wajumbe, au watu juu ya mnara, wanaopanda juu katika Roho, mbali zaidi ya taratibu zote, na mabomu yote ya atomiki, na tafiti za kisayansi. Anao watu ambao wameumbwa maalum kwa kusudi hilo, wanaopanda kwenye ngome za Kalvari, katika Jina la Bwana Yesu, na kusimama juu ya msalaba, nao wanaweza kurudisha Ujumbe, "BWANA ASEMA HIVI." Macho yao ya kiroho yana uwezo mkubwa sana kuliko makuhani hekaluni; kuliko ya mtu wa kawaida katika wito wa maisha; kwa maana wameumbwa maalum kwa ajili ya kazi ambazo Mungu amewaitia. Kwa hiyo, inatupasa kuwa waangalifu tunaposikia juu ya mambo yanayokaribia.

⁴⁰ Ndipo ningebadilisha sasa kwa muda mfupi tu. Na kuelekeza usikivu wenu kwa Mfalme wa tai hawa, au manabii, au walinzi wa minara. Huyu ni Bwana Yesu, Mwenyewe. Nayo siku hii tunayoishi ilikuwa kubwa sana kuliko siku ambayo Yeye alikuwa hapa, mpaka, alipokuwa moja kwa moja katika vivuli vya msalaba, Yeye alinena zaidi juu ya Kuja Kwake mara ya pili kuliko alivyonena juu ya kuondoka Kwake. Ukiyachunguza Maandiko kwa makini, utaona kwamba kabla tu ya kuondoka Kwake, kwamba alitabiri juu ya mambo ambayo yangetukia katika siku hii.

⁴¹ Alijua kwamba hana budi kusulubiwa. Alijua kwamba hana budi kuteseka a—asiye na hatia kwa ajili ya wenye hatia. Alijua ya kwamba angefufuka tena kutoka kaburini, siku ya tatu. Alijua ya kwamba hapakuwapo na nguvu zozote ambazo zingeweza kumshikilia kaburini, kwa maana Neno la Mungu lilikuwa limesema, “Sitamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu.” Wala hapakuwapo na nguvu ambazo zingeweza kuvunja unabii huo. Neno Lake litakuwa kweli, nayo yatatimizwa katika majira Yake. Naye alikuwa na matumaini ya kwamba, yale Baba alikuwa amesema, Baba aliweza kulitimiza Neno Lake.

⁴² Kwa hiyo, moyo Wake mkuu uliokuwa ndani Yake, ambao ulikuwa ndio Kiti cha Enzi cha Mungu, moyoni Mwake alijua ya kwamba nyakati hizi kuu za majaribu zingekuja kuyajaribu mataifa yote, na kuwajaribu watu wote. Kwa hiyo, basi, alijua ya kwamba swali kuu lilikuwa, si kama Yeye angefufuka tena, ama kama angesulubiwa kulingana na Maandiko Matakatifu, au si kama angepaa Juu, na Roho Mtakatifu angekuja. Lakini swali lilikuwa, “Je, kutakuwa na imani yoyote iliyosalia duniani katika Kuja Kwake?” Nayo imani huja wapi? “Kwa kusikia Neno la Mungu.” Hilo lilikuwa ndilo swali Lake. “Je, kutakuwako na imani duniani nitakapokuja?” Je, atakuta watu wanaoamini Neno Lake?

⁴³ Sasa wakati sisi, katika siku tunayoishi, tunaweza kufungua kurasa za Neno Lake lililobarikiwa, na kuyaona mambo yale yale aliyosema yangetukia, yakikaribia duniani siku hizi, ishara na maajabu yanafanyika: “Watu wanavunjika moyo kwa hofu.” Kuna “mshangao wa wakati na dhiki kati ya mataifa. Mambo ya kutisha angani,” kama visahani virukavyo, na Pentagon yote ikitikisika. “Na bahari ikivuma, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Watu wakivunjika moyo kwa hofu.” Silaha kubwa za atomiki zimewekwa, zikingojea. Utusitusi ukining’inia juu ya dunia, ambao ulimwengu haujawahi kushuhudia hapo awali.

⁴⁴ Juma lililopita nilikuwa na fursa ya kuzungumza na mmoja wa marafiki na ndugu zangu wapendwa, Kapteni Julius Stadslev, aliyeandika kitabu, *Nabii Azuru Afrika*. Naye Ndugu Julius alikuwa California, ambako sasa anachukua masomo yake ya umeja jeshini. Naye... Wao, watumishi wa majeshi,

walimpeleka kwenye mahojiano makubwa. Nao wakaichunguza nasaba yake hata ilibidi wathibitishe hata mama wa nyanya yake alikuwa ni nani, na historia yao na jinsi walivyokuwa, kabla hajaketi katika mkutano huu.

⁴⁵ Ndipo alipotoka mkutanoni akapanda juu ya kilima tulipokuwa tukikaa pamoja na baadhi ya marafiki, alikutana nami huko nje chini ya mremu, naye akasema, “Ndugu Branham, ndicho kitu cha kudhoofisha sana ulichowahi kusikia.” Akasema, “Niko chini ya viapo vingi sana hata nisingeweza kusimulia, au nisingeweza kutoa habari yoyote,” kasema, “kwa sababu tunaninii... Walitupapisha kiapo kizito. Ila,” kasema, “Naweza kusema hili. Jeshi litakoma. Hawatakuwa na jeshi tena; walinzi wachache tu kote. Hawatakuwa na jeshi la angani tena. Ha—hawatakinia kuunda ndege zierendazo kasi zaidi na kadhalika, isipokuwa ziwe ni kwa matumizi ya kibiashara tu. Wanamakinia mvuto mmoja tu wa chombo cha kufyatulia. Kutatokea maangamizi makuu.”

⁴⁶ Akasema, “Ndugu Branham, umma haujui jinsi siri za mambo ya kijeshi zilivyo.” Akasema, “Wakati maofisa hawa wakuu walipozungumza chumbani,” akasema, “kulitokea utusitusi wa kutisha sana mle chumbani, mpaka mmoja wa wanasayansi wao wakuu akasimama, na kusema, ‘Laiti ningaliweza kuchukua mkokoteni wa kale pamoja na ng’ombe, na kwenda huko nyuma ya milima, na kujipandia kijishamba cha kabichi na maharagwe, na kusahau yote juu yake.’ Loo,” akasema, “ingetukia, kama habari hizi zingeufikia umma, ulimwengu mzima ungekumbwa na hofu ya ghafla. Hatari inakaribia.”

⁴⁷ Akasema, “Hawana budi... wanawaondoa watumishi wao sasa kutoka visiwani. Wanaondoa vikosi vyao Uingereza. Nao wana mashua kubwa zilizowekwa huko nje, zenye aina fulani za silaha. Na wanangojea tu mrusho wa kwanza wa kombora, na kila taifa litayavurumisha kwa wakati mmoja.” Kasema, “Hakutakuwa na chembe moja ya majani iliyosalia duniani, wala mlima mmoja ambao hautaporomoshwa chini. Nayo yanaweza kutokea wakati wowote.” Loo, ni saa ya huzuni iliyoje!

⁴⁸ Na mambo haya yote mnayosikia kuhusu visahani virukavyo. Nanyi mliyasikia yale mahojiano na mtu yule, nadhani, jana, kwenye radio, anayedai kwamba alizungumza na watu. Sitaki kumpuuza mtu huyo, lakini mfumo wake wote ni kinyume na Neno. Sio kweli. “Na ati kwenye sayari ya Marsi, hawana mauti, nao wamekuja hapa kutufundisha jinsi ya kutokuwa na mauti.” Lakini ilipofikia kwenye uthibitisho, hakuwa na chembe moja ya uthibitisho, ambao angeweza kulithibitisha. Wazo fulani tu la kubuni ambalo alikuwa ametunga. Na, nionavyo mimi, ni uongo, kwa sababu Biblia ilisema tofauti na yale aliyosema.

49 Huenda nikaelezea ninachowazia kuhusu visahani virukavyo. Siamini kwamba ni vivuli. Siamini kuwa ni za kubuni. Ninaamini. . . Wala hii hailifanyi kuwa kweli. Ni wazo langu tu. Bwana hajaniambia hivi ndivyo vilivyo. Lakini, kwa kuyaangalia Maandiko, kwa kuwa Hapo ndipo tunapopata mambo yote.

50 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Na kabla ya maangamizi ya Sodoma, na moto kushuka na kuuteketeza mji na nchi tambarare, kulikuweco na Malaika waliotumwa kutoka Mbinguni, ambao waliangalia ndani na kuchunguza, waone kama mambo haya yalikuwa kweli au la. Basi si ingekuwa tu ni kama Mungu kuwatuma tena Malaika Zake wakachunguze wapate kujua, kabla tu ya yale maangamizi makuu kuja? Basi mliona? Kulikuwako na Malaika mmoja aliyekuja, Yule aliyemtembelea mzee mmoja ambaye alikuwa amekata kauli kwa ajili ya Mungu, na alikuwa akiishi, akidharauliwa na walimwengu, katika hema huko jangwani, kwa sababu mtu fulani alikuwa amechagua na kuchukua mali yake yote. Lakini akasema, “Hiyo ni sawa. Nitakaa tu hapa katika mapenzi ya Mungu.”

51 Afadhali niwe katika mapenzi ya Mungu kuliko kuwa na pesa zote ambazo ulimwengu unaweza kukugawia.

52 Na mara tu kauli hiyo ya mwisho ilipokatwa, ndipo Malaika wa Bwana alipomjia Ibrahimu na kusema, “Angalia mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini. Yote ni yako, Ibrahimu.”

53 Maandiko yanatwambia, “Heri wenye upole: maana hao watairithi nchi.” Inaleta tofauti gani? Vitu vyote vya ulimwengu vitaangamia pamoja na ulimwengu, lakini Mungu kamwe hawezi kuangamia.

54 Nami ninaamini kama vile, ninavyoongozwa kuamini, yaani, ikiwa ile picha ya Malaika wa Bwana Yule ajaye na kufanya upambanuzi. . .

55 Je, ulimwona Malaika Yule aliyemjia Ibrahimu? Alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, alipokuwa akizungumza na Ibrahimu, na kusema, “Nitaitimiza ahadi Yangu kwako.”

56 Loo, ni Ujumbe wa jinsi gani wa Malaika wa Mungu katika siku hii, Yule ambaye ataitimiza ahadi Yake! Kutokuamini kwote kwa ulimwengu, wenye kushuku, wasiosadiki uungu, na makafiri, na wasioamini, kamwe hawatazitangua Nguvu za Mungu. Itatokea vivyo hivyo tu.

57 “Nitakumbuka ahadi Yangu, na nitaitimiza ahadi Yangu.” Ndipo Sara akacheka hemani nyuma Yake.

58 Na huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, akasema: “Kwa nini Sara akacheka?”

59 Ndipo Sara akatoka nje haraka na kusema, “Sikucheka,” kwa sababu aliogopa.

60 Huyu alikuwa ni Mtu wa aina gani? Unashangaa ni Mlinzi wa aina gani aliyekuwa kwenye mnara wakati huo? “Huyu ni mtu wa aina gani aliye pamoja nasi, huku mgongo Wake umeelekezwa kwangu, na bado alijua ya kwamba nilicheka, ndani ya hema?” Kumbukeni, Yeye alikuwa ni Mlinzi.

61 Naye akageuka, akasema, “Naam, ulicheka.” Naye aliogopa.

62 Sasa, tunaona tena, ya kwamba katika siku hii kabla tu ya Kuja kwa Bwana, Viumbe vivi hivi vitarudi tena. Nami nashangaa, tunapotazama huku na huku na kuona tabia Yao, tunaangalia yale wanayofanya, nami nashangaa kama nyingi ya tamasha hizi za ajabu siyo hasa yale ambayo Yesu alisema yangetukia. “Kutakuwa na ishara mbinguni juu. Na duniani kutakuwa na dhiki kati ya mataifa, mshangao wa wakati, matetemeko ya nchi mahali mahali, na wanaume wakifa kwa ugonjwa wa moyo.” Si wanawake; wanaume. Wanawake hawafi mara nyingi kwa ugonjwa wa moyo. Ni wanaume. Inatimiza kile ambacho Yesu alisema kingekuwako. Ni vile hasa Yeye alivyosema ingekuwa.

63 Na basi kama tungeweza kuendelea, saa baada ya saa, juu ya manabii wote, jinsi ambavyo wametabiri juu ya siku hii. Je, haitamfanya mtu alie, “Mlinzi, habari gani za usiku?”

64 Pentagon haina jibu. Marekani haina jibu. Ujerumani, Urusi, hakuna hata moja yao iliyo na jibu. Sayansi haina jibu.

65 Ni nani aliye na jibu? Mlinzi, aliye juu ya ukuta, ana jibu. “Mlinzi, habari gani za usiku?” Naye Roho Mtakatifu ndiye Mlinzi huyo anayewatayarisha watu, na kutoa maonyo kutoka kwa Mungu. Amewekwa kama Mlinzi. Tunaona wagonjwa wakiponywa, macho yaliyopofuka yakifumbuliwa, masikio ya kiziwi yakizibuliwa, viwete wakitembea, viwete wakivuja... wakirukaruka kama ayala. Kutimiza... Ni kitu gani? Ni Kuja kwa Bwana, kukipenyeza.

66 Na mambo haya yote, na maonyo haya! Na watu wanaendelea kusonga mbele hadi kwenye karamu zao za bia, mpaka nyakati zao za upumbavu. Na wanafanya mizaha. “Na wanacheza, na wanakula, na wanakunywa, na wanaoa, na wanaolewa,” kama vile tu Mungu alivyosema itakuwa. Hakuna njia ya kuwazuia.

67 Basi ukiangalia, katika wakati huu mkuu wa kanisa, kulingana na Ufunuo 3, katika wakati huu sasa ndio uliopewa Nyota ya Asubuhi, kabla tu ya kule Kuja.

68 Tazama jinsi Isaya alivyokuwa wa Kimaandiko aliposema, “Mlinzi, habari gani za usiku?” Akasema, “Asubuhi inakuja, na usiku pia.” Ati nini? Asubuhi inakuja, lakini usiku unaitangulia asubuhi. Ilikuwa ni nini? Mtu yeyote anajua kwamba kabla tu ya

mapambazuko, kwenye zile saa tu za kukaribia mapambazuko, inakuwa giza kuliko ilivyowahi kuwa.

⁶⁹ Loo, marafiki zangu, sikilizeni BWANA ASEMA HIVI. Ikiwa mnanihesabu kuwa mtumishi Wake, ni kabla tu ya mapambazuko. Ndiyo maana utusitusi huu wa kutisha uko juu ya dunia. Ni kabla tu ya Kuja kwa Bwana Yesu. Hakuna tumaini zaidi lililosalia katika kitu chochote ila Kuja Kwake.

⁷⁰ Mataifa yanapigana na mataifa. Na wamejipumbaza kupitia kwenye maabara ya Mungu mpaka wamepata nguvu za kulipuana wakawa majivu ya atomiki. Nao ni waovu, na ni wakosa dini, na hawafanani na Kristo. Na nia pekee waliyo nayo, na lengo, ni kuangamiza. Nao wamevuviwa na malaika mwangamizi aliyetumwa kutoka mbinguni ili kuwavuvia watu hawa.

⁷¹ Acha niseme, katika Jina la Bwana Yesu, Roho Mtakatifu ametumwa kama Mlinzi kwenye mnara. Huku watu wakilia, “Habari gani za usiku?” Je, umechoka na maisha haya? Je, umechoka na dhambi? Je, umechoka na misafara ya mazishi, na magonjwa, na uovu kila mahali? Usiku umekuwa mrefu na wa kuchosha? “Habari gani za usiku, Mlinzi?”

Akasema, “Asubuhi inakuja.” Unaona faraja?

⁷² “Na usiku unakuja pia.” Usiku ni nini? Angalia jinsi Isaya alivyokuwa katika upatanifu mkamilifu na Maandiko. Katika mwenendo wa kawaida wa—wa maumbile, ni kwamba sikuzote kukaribia kwa jua hugandamiza giza pamoja na kulifanya jeusi. Kuna giza zaidi kabla ya mapambazuko kuliko wakati mwingine wowote usiku. Kwa nini? Mwanga unaokaribia ndio ambao unafanya giza.

⁷³ Pia ni kule kukaribia kwa Bwana Yesu sasa ndiko kunaleta utusitusi huu juu ya nchi. Je, hakusema, “Mambo haya yaanzapo kutokea, inueni vichwa vyenu kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia?”

⁷⁴ Palestina ni taifa. Wayahudi wamerudi kutoka kote duniani, nao wamewekwa kule wapate kumwona Yeye akija, kama Mungu alivyosema wangepanya. “Jifunzeni mfano wa mtini, unapotoa machipukizi yake.” Alisema, “Ndivyo itakavyokuwa kwamba kizazi hiki hakitakwisha, hakitamalizika, hakitafika mwisho, mpaka mambo haya yote yatakapotendeka.” Kizazi gani? Kizazi kitakachouona mtini ukitoa machipukizi yake. Israeli daima imekuwa ndiyo mtini.

⁷⁵ “Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu,” alisema Yoeli. “Yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na tegu. Na yaliyosazwa na tegu, yameliwa na nzige.” Na ikiwa utaangalia, huyo ni mende yule yule. Kila mmoja wa wadudu hao anayeendelea kuula huo mti, ni mdudu yule yule, ila tu katika hatua tofauti. Na dhambi ile ile na kutokuamini kulikoanza kuwatafuna Wayahudi, kwamba, “Yesu hakuwa Kristo,” waliula

mti huo ukawa kisiki kitupu. Ndipo nabii akaona hilo, naye akalia. Lakini Bwana akasema, “‘Nitarudisha,’ asema Bwana, ‘miaka yote iliyoliwa na madumadu, na nzige, na tunutu.’”

⁷⁶ Na kwa mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili mia tano, Wayahudi wanarudi katika nchi ya uenyeji wao. “Kizazi hicho hakitabatilika, hakitapita, mpaka mambo haya yote yatimie.” “Ndipo nitaimwaga Roho Yangu katika siku za mwisho,” asema Mungu, ‘juu ya wana na binti Zangu, nao watatabiri. Nami nitaonyesha maajabu.’”

⁷⁷ Wagonjwa wanaponywa, nguvu kuu zinafanyika, kwa Roho yule yule aliyeketi na angeweza kumwambia Ibrahimu ya kwamba Sara alicheka chumbani nyuma Yake.

Ndipo tunapaza sauti, “Mlinzi, habari gani za usiku?”

⁷⁸ Naye akasema, “Usiku unakuja.” Tazama. Usiku, kwanza . . . Asubuhi inakuja, kwanza. Kisha, usiku, pia.

⁷⁹ Kabla tu ya mapambazuko, daima kuna nuru moja kuu ambayo sikuzote huwekwa mbinguni, na hiyo ni nyota ya asubuhi. Unapooni nyota ya asubuhi ikiendelea kung’aa, zaidi na zaidi, ndipo dunia inakuwa giza zaidi na zaidi. Na sababu ya kung’aa zaidi, ni kwamba dunia ina giza zaidi.

⁸⁰ Nalo Kanisa la siku hizi za mwisho, Mwili wa Kristo ulioteuliwa na kuitwa utoke, limeahidiwa na Biblia ya kwamba angewapa ile Nyota ya Asubuhi.

“Mlinzi, habari gani za usiku? Itakuwaje?”

⁸¹ Hili hapa. Maangamizi kamili yanakuja kwa ulimwengu wote. Lakini kabla ya maangamizi hayo kutukia, Kanisa la Yesu Kristo litaenda katika Unyakuo, kumlaki Bwana Wake.

⁸² Nyota ya asubuhi itafanya nini? Ni kitu gani kinachofanya nyota kung’aa sana wakati huo? Ni kukaribia kwa jua. Nyota ya asubuhi inauakisi mwanga wa jua. Nyota zingine zinaonekana kufifia kwenye wakati huo.

⁸³ Theolojia zote za kujibunia, kutojali kwote baridi, kwa kawaida kutakauka. Lakini yule mlinzi anayeketi kule juu ya mnara, pamoja na Nyota ya Asubuhi, ataakisi Ujumbe wa kweli wa Bwana Yesu unaokaribia hivi karibuni, kwa sababu Yeye ni mwangavu zaidi na zaidi, wakati wote, wakati jua linapozama kuchomoza.

⁸⁴ Loo, ningesema, nyota za asubuhi, inukeni mkaangaze kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa maana kukaribia kwa giza la usiku wa manane kuko juu ya dunia, na giza kuu juu ya watu. Lakini asubuhi inakuja, na nyota zinapaswa kutoa nuru zao.

⁸⁵ Wazia juu ya hiyo saa ya kutisha ambayo inaukabili ulimwengu wote. Wazia juu ya utusitusi huo wa kutisha ambao unamkabili kila mtu ambaye hajaokoka siku hizi. Mataifa yote, na milima yote, na mashamba yote na nyumba

zote walizojitukuza nazo, zitafanywa unga, zitakuwa majivu ya volkeno tena, kwa dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho.

⁸⁶ Lakini wale wanaompenda Bwana, wale walio na Nuru ya Nyota ya Asubuhi, kwamba wanaelekeza—wanayaelekeza macho yao Kwake, na kuyaondoa kwenye mambo ya ulimwengu! Na kama vile Paulo alivyoandika katika waraka wake wa kumalizia, kabla hajaondoka duniani, alikuwa mchovu, na mwenye wasiwasi, na amechoka. Loo, jinsi ninavyomhurumia maskini yule Myahudi. Aliposema, “Mtu asinisumbue. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, na mwendo wangu nimeumaliza. Imani nimeilinda. Na tangu sasa kuna taji ya haki ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki atanipa siku hiyo.” Kisha akawazia juu ya kuja kwa nyota za asubuhi, akasema, “Si mimi tu, bali na wote wanaompenda kuonekana Kwake.” Loo, “Inueni vichwa vyenu, ukombozi wenu unakaribia.”

⁸⁷ “Mlinzi, ni kitu gani kinacholifanya gazeti kusema hivi? Ni kitu gani kinachoifanya sayansi kuogopa kusogea? Ni kitu gani kinachoifanya Pentagon kuogopa kutoa hii habari nje?” Kwa sababu watu wangejiua na kutupa pesa zao mitaani, na kadhalika. “Ni nini... Kuna nini? Ni nini? Kuna habari gani za usiku?”

⁸⁸ “Asubuhi inakuja.” Hiyo ni kweli. Yote yanahusu nini? Ni kufanyizwa kwa asubuhi, kuja, na inasukuma Nuru mbele. Inafanya giza kuu kuja kabla tu Nuru haijaanza kuangaza.

⁸⁹ Nina furaha sana kuwa Mkristo. Nina furaha sana kwamba mimi ni mlinzi Wake, mmoja wao, ambaye amesimama ukutani, akipaza sauti, “Jiwekeni tayari kumlaki Mungu, kwa kuwa saa ya Kuja Kwake inakaribia.”

⁹⁰ Nanyi, hapa katika kanisa hili asubuhi ya leo, kama kuna mmoja ambaye hana hakika ya kwamba ile Nyota ya Asubuhi inaangazia Nuru Yake moyoni mwako, yule Roho Mtakatifu mkuu, naomba ujiandae kwa ajili ya jambo hilo. Kwa maana hilo hapo tukio moja kuu sana lililowahi kutukia, limekaribia sasa hivi. Tumesimama ukingoni, tukitazama mchezo wa kuigiza ukiandaliwa.

⁹¹ Mara nyingi nimeangalia sinema, jinsi ambavyo huko Hollywood na katika sehemu mbalimbali, wakiandaa michezo yao ya kuigiza. Na jinsi wanavyowachukua nyota wao, na kadhalika wao, na kuwafanya nadhifu. Na jinsi wanavyowafunza na kila kitu kabla ya mchezo mkuu wa kuigiza kufanyika. Daima ninastaajabia kuutazama, na nikijua ilibidi iwe ni bandia.

⁹² Vitu vyote bandia hutengenezwa kutoka kwa vitu halisi. Hakuwezi kuwa na dola bandia kusipokuwapo na ya kweli. Hakuwezi kuwa na mnaifiki kusipokuwa na Mkristo halisi.

Hakuwezi kuwa na ujumbe wa uongo kusipokuwa na wa kweli. Hakuwezi kuwa na usiku kusipokuwa na mchana. Bila shaka!

⁹³ Na nilipokuwa nikiwatazama wakiandaa michezo yao ya kuigiza, nami nimewazia, “Loo, tumesimama mbali sana juu ya mnara, mbali kuliko kitu chochote kile katika ulimwengu huu, nasi tunaangalia mambo mawili makubwa kuliko yote; kule kuisha kwa wakati, na kule Kuja kwa Bwana.” Hivi karibuni, “Hakutakuwako na wakati tena.” “Hakutakuwako na wakati tena,” na kule Kuja kwa Bwana.

⁹⁴ Naye mpinga-Kristo, ana raia wake wanaoketi pale. Ana ukomunisti. Ana itikadi mbalimbali: ana ukanisa, ana Ukatoliki, ana Uprotestanti. Ameandaa kila kitu, ili kufanya maonyesho makubwa.

⁹⁵ Lakini nina furaha sana ya kwamba kuna Baba Mbinguni, Ambaye amewaandaa wahusika Wake, pia, kwa ajili ya mchezo huu mkuu wa kuigiza. Wakati mpinga-Kristo anapowapeleka kwenye mauti haya ya kila kitu, hata ya wakati, Mungu yuko tayari katika mchezo Wake wa kuigiza kuliinua Kanisa Lake hadi katika Umilele, katika milki za upeo wa furaha za Milele, pamoja na Mungu Mwenyewe. Wakati, maskini miili hii miovu itakapobadilishwa na kufanywa kama Mwili Wake Mwenyewe mtukufu, na uharibifu huu utakapochukua kutokupatikana na mauti, na katika mfano Wake tutasimama milele.

⁹⁶ Tazameni! Ninyi mnaotazama televisheni, ninyi mnaosikiliza redio, ninyi mnaosoma magazeti yenu, ninyi mnaopenda kusikia habari na mnashangaa hii ni nini, isikilizeni sauti yangu: “Asubuhi inakuja, na usiku unakuja pia.” Asubuhi inawajia wale walio tayari kwa ajili ya asubuhi, nao usiku unawajia wale ambao hawajajiandaa kwa ajili ya asubuhi. Mungu na aiandae mioyo yetu leo hii.

⁹⁷ “Kwa maana asubuhi itapambazuka ya Milele yenye kung’aa na nzuri.” Na kama mshairi alivyosema, “Watu wake waliochaguliwa watakusanyika makazini mwao ng’ambo ya anga. Majina yaitwapo huko ng’ambo, nitakuwako.”

Na tuombe.

⁹⁸ Katika saa hii ya utusitusi juu ya nchi, na maangamizi kila mahali, Bwana Mungu, tuko. . . Kamwe hatuwezi kuelezea jinsi tunavyojisikia, na shukrani na furaha mioyoni mwetu, ya kwamba Yesu Kristo alishuka kutoka Utukufuni, na akafanyika mtu kama sisi, akakaa miongoni mwetu. Na ndipo alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, akaja kupitia njia ya Paradiso, na kuzichukua nafsi zinazongojea, akavunja kila nguvu za kiroho ambazo ibilisi alikuwa ameifunga dunia kwake, na kufanya mstari, ili nuru ya jua ya neema ya Milele ya Mungu ipate kuangaza juu ya wale ambao wako tayari kuipokea.

⁹⁹ Mungu, jalia leo, kwamba watu kila mahali wataharakisha, wafanye hima, waingie katika Ufalme, kwa maana Ujumbe

sikuzote umekuwa wa dharura. “Hima, hima, tokeni!” yule Malaika alisema, kule Sodoma, “Siwezi kufanya lolote mpaka ufike huku.” Bwana, jalia, kwamba ingawa Ujumbe umejaa neema, na nguvu, na upendo, hata hivyo ni wa dharura. Jalia, Bwana, ya kwamba watu waje upesi na kumpokea Kristo na kujazwa na Roho Mtakatifu. Kwa maana Yesu alisema, “Walio wa Mungu, husikia Maneno ya Mungu.” Jalia waje wakatubu dhambi zao, wakabatizwe katika Jina la Bwana Yesu, kwa ondoleo la dhambi zao, na kujazwa na Roho Mtakatifu; kuweka nafsi zao katika hali ambayo kanisa la kwanza lilikuwa nayo, ndivyo itakavyokuwa wakati Wewe utakapokuja.

¹⁰⁰ Tunashukuru kwa ajili ya Ujumbe, na kuomba ya kwamba Wewe utaubariki, Bwana, kwa ajili ya wema na mioyo yetu, tunapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

¹⁰¹ [Sehemu tupu kwenye kanda. Mpiga piano anaanza kucheza *Watakapopiga Zile Kengele Za Dhahabu*.—Mh.]

Moja kwa moja tutafika langoni,
Tukaishi huko pamoja na wasiopatikana na
mauti,
Watakapozipiga hizo kengele za dhahabu kwa
ajili yako na yangu.

¹⁰² Je, hamumpendi tu Yeye? Sasa, ujumbe umekwisha, hebu na tumwabudu tu namna hiyo, katika Roho. Ninii tu. . . Yuko hapa. Maneno makuu, makali, bali ni kweli. Ninayanena katika Jina la Kristo. Kukaribia kwa ile siku. Ikiwa mwaniheshimu. . . nataka huu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . wewe na mimi.

Hebu tuinue tu mkono wetu juu.

. . . husikii. . .
Husikii Malaika wakiimba?
Ni Yubile tukufu haleluya.
Katika huko mbali kutamu milele,
Ng'ambo tu ya mto unaong'aa,
Watakapozipiga hizo kengele za dhahabu kwa
ajili yako. . .

¹⁰³ Wakati akiendelea kuucheza huo, hebu tupeane mikono na mtu aliye karibu nawe! . . . ? . . .

. . . tamu milele,
Ng'ambo tu. . .
Wakati. . . fika tu kwenye huo ufuko kwa
imani. . .

¹⁰⁴ Semezaneni tu, “Msafiri, nina furaha sana kuwa pamoja nawe.”

. . . moja tutafika langoni,
Tukaishi kule pamoja na wasiopatikana na
mauti,
Watakapozipiga kengele hizo za dhahabu kwa
ajili yako na yangu.

Je, husikii kengele sasa zikilia?
Huwasikii Malaika wakiimba? (Ni nini?)
Ni Yubile tukufu haleluya.
Katika huko mbali sana kutamu milele,
Ng'ambo tu ya mto unaong'aa,
Watakapozipiga hizo . . .

¹⁰⁵ Hiyo ilinikumbusha tu jambo fulani. Mke wangu, kule nyuma, anakumbuka jambo hilo vizuri. Nilikuwa na majaliwa ya kutembelea kanisa la kale la Pisgah, taasisi ya Biblia huko California. Nilikuwa na ibada ya usiku mmoja pamoja nao. Hicho ndicho kituo asili cha kale cha nguvu. Mahali pazuri jinsi gani! Nilikutana na huyo mchungaji, Ndugu Smith. Mnajua, wanachapisha gazeti. Wana msaada. Hawachukui sadaka. Kila kitu ni bure. Nao wamekuwepo kwa muda wa miaka hamsini na kitu. Ilianzishwa na daktari ambaye alikuwa kiwete, aliyekuja California apate usaidizi. Daktari akasema, "Hakuna kinachoweza kufanywa kwa ajili yako."

Ninaamini ilikuwa ni marehemu Dk. Price ama mtu fulani, aliyemwombea, chumbani asubuhi moja. Hakupata matokeo yoyote, inaonekana, papo hapo. Hilo halimaanishi chochote. Kwa hivyo, akaanza kutoka. Akasema, "Kwa namna fulani, nyingine, ninaamini, hata hivyo." Ndipo alipoanza kutoa mguu wake kutoka kwenye teksi, mguu wake uliolemaa ukakunjuka. Akaanzisha Makazi ya Pisgah.

¹⁰⁶ Hivi majuzi usiku nilikuwa kule, nikihubiri. Walikuwa wamesongamana katika jumba hilo kubwa la mikutano, na mamia mara mamia wakisimama kote barabarani na kadhalika, ambapo walienda nyuma. Ndipo baada ya Ujumbe kumalizika, jambo fulani likatendeka, mambo mawili ambayo sikuwahi kushuhudia hapo awali maishani mwangu. Hawakuwa tu ni kundi la watu wanaopenda kupiga kelele nyingi. Hawakuwa kundi la watu walioketi, wamekauka. Walikuwa ni watu waliojazwa na Roho. Nami nilifurahia ushirika huo wa ajabu. Ndipo tulipokuwa . . .

¹⁰⁷ Kabla tu sijaanza kuwaombea wagonjwa, walianza kuimba kitu kitamu namna hiyo. Nami nikasimama, nikastaajabu. Nikasema, "Kuna kitu kinachoendelea hapa. Sielewi." Nikasikiliza tena, ndipo nikasikia kwaya mbili. Nikasema, "Hapana shaka kuna kasoro." Nami nikatikisa kichwa changu. Na, kwa masikio yangu, tena. Nikasema, "Ee Bwana, labda ni kurudishwa mwangwi kwa sauti ya kwaya hii *hapa*." Ninasikia nyingine *hapa* juu, juu sana, vigongo vya juu sana. Nikasema,

“Lazima iwe ni hapo juu.” Kwa hiyo nikatoka kwenye kiti cha wahudumu, hadi hapa roshani ya kwaya. Ilikuwa ni huko juu.

Nami ni—nikamwambia mke wangu, nikasema, “Unaisikia hiyo, mpenzi?”

Alisema, “Ni nini hiyo?”

“Dada Arganbright,” Nikasema, “unaisikia hiyo?”

Akasema, “Ndiyo. Nimeisikia mara moja hapo awali, maishani mwangu.”

Nikamwendea Ndugu Arganbright, “Je, unaisikia hiyo?”

“Naam.”

¹⁰⁸ Kila mtu ameinamisha vichwa vyao, wakiimba. “Loo,” nikasema, “labda . . . Na—nataka kuwa na uhakika. Sitaki kuwa na shaka, lakini, Bwana, kama mimi ni shahidi Wako, ikiwa nitakuwa mlinzi, sina budi kujua ninachozungumzia. Sina budi kuwa na uhakika na hili.”

¹⁰⁹ Kama vile uponyaji wa Kiungu, kama sina uhakika, sitasema lolote juu yake. Kama sina hakika huku ni Kuja kwa Bwana, nisingesema lolote juu yake. Sina budi kuwa na uhakika.

¹¹⁰ Nilirudi tena kwenye shimo. Kila mtu ameinamisha vichwa vyao.

¹¹¹ Na ule wito wa madhabahuni, watu wengi walielekeza mikono yao dirishani, wakimjia Kristo. Nao walikuwa wakiimba. Nilipofika hapa chini, nilisema, “Bwana, haiwezekani. Watu hawa wanaoimba *hapa* chini walikuwa ni watu wa kawaida tu, lakini hii *hapa* juu ilisikika kana kwamba walikuwa ni wachache . . . Labda elfu mbili ama tatu wakiimba, *hapa*, lakini ilionekana kana kwamba labda kungekuwa na laki moja *huko* juu.” Na ilikuwa mojawapo ya sauti tamu sana, soprano ya juu kweli, kama sauti za wanawake. Nikasikiliza, na mitetemeko ikapitia tu kote mwilini mwangu.

¹¹² Nilirudi nyuma tena kwa dakika moja tu. Nikasikiliza. Nikapanda juu, juu sana. Nikarudi, maana waliendelea tu kuimba katika Roho. Nikasikiliza tena. Haikuwa ni sauti *hii*. Niliweza kuzisikia *hapa* chini, aina moja ya sauti; na hii *hapa* juu, aina nyingine ya sauti.

¹¹³ Basi ibada ilipokwisha, nikamwambia mchungaji, “Mchungaji, nilisikia kitu cha kigeni.”

Kasema, “Ilikuwa ni nini, Ndugu Branham?”

¹¹⁴ Nikasema, “Nilisikia sa—sauti za soprano za wanawake, katika sauti zilizofunzwa sana, za kupendeza sana nilizopata kusikia maishani mwangu, *mle* ndani.”

¹¹⁵ Akasema, “Zimesikika hapa mara nyingi, Ndugu Branham.”

¹¹⁶ Nilikuwa nimesoma juu ya mama mzee . . . Loo, nasahau jina lake sasa, aliyekuwa akiwaombea wagonjwa. Ndipo usiku

mmoja baada ya mchungaji kufunga mahubiri yake, maskini huyo mama alishuka kuwaombea wagonjwa. Alikuwa na watoto wadogo watano ama sita, karibu naye. Ndipo akasimama na kusikiliza. Na ni Bibi Woodworth-Etter, kama nyote mliwahi kusoma kitabu chake. Naye akasikia, akasema, “Kwaya fulani inaimba juu ya uimbaji kanisani.”

Baada ya hizo sauti kunyamaza, *hapa* chini, Hizo zinaendelea kuimba, mnaona. Nami nikasimama pale.

¹¹⁷ Na papo hapo, huko nyuma ya jengo kabisa... Mnaona jinsi ilivyo na utaratibu, kamilifu? Sasa, na—naamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini ni karama ya Mungu, iliyomo kanisani. Ninaamini imetumiwa vibaya kama vile Maandiko mengine yametumiwa vibaya, lakini kuna iliyo halisi. Naam. Ndipo mtu huyu akasimama nyuma ya jengo, huko nyuma kabisa, naye akasema kama maneno manne ama matano katika lugha nyingine. Sio—sio tu ninii... Ilikuwa la—lahaja. Ungeweza kusikia. Kila mtu alikuwa kimya.

¹¹⁸ Ndipo kitu Fulani kikanijia, sikupata kufasiri maishani mwangu. Wala sikuitumia wakati huo, maana nilikuwa naogopa. Mambo hayo ni ya Mungu. Afadhali usijipumbaze nayo.

¹¹⁹ Ndipo kitu Fulani kikaniambia, “Mchungaji ataomba maombi ya imani.” Ilinibidi kufunga kinywa changu. Ndipo nikasubiri. Na hili hapa likaja tena, wimbi likinijia, na kusema, “Mchungaji ataomba maombi ya imani.”

¹²⁰ Nikawazia, “Bwana, sina karama za ufasiri. Yangu ni kuwaombea wagonjwa, kwa hiyo sina karama za ufasiri.” Nami nikafunga kinywa changu tena na kusimama kimya.

¹²¹ Na papo hapo tu mchungaji akasimama na kuanza kuwaombea wagonjwa. Loo, Yeye ni Mungu! Ugonjwa uliponywa, kotekote jengoni, kila mahali. Ni nini? Mapambazuko. Bado kuna tawi dogo lililosalia. Msijali. Mungu hajawahi kuwa bila shahidi.

¹²² Nikitumaini sasa kwamba mtu fulani wa kiajabu sana, mahali fulani, labda si kwa sauti ya Kimalaika, lakini kitu fulani kitakachomfanya kila mwenye dhambi, kama kuna watu kama hao humu jengoni, ajue kwamba usiku unazidi kuingia giza zaidi na zaidi juu ya nchi, na giza kuu. Lakini Kuja kwa Bwana kunakaribia, ndiko kunakosababisha jambo hilo. Na kama mlinzi wenu, ningesema, “Asubuhi inakuja.” Iweni tayari, enyi nyota za asubuhi, angazeni!

¹²³ Je, ni wangapi wangependa kukumbukwa katika maombi ya kufunga kabla hatujaenda? Inua tu mkono wako.

¹²⁴ Mungu Mpendwa, unawaona watu wanapoinua mikono yao. Nao ni waaminifu katika hili. Wengi wa wale wanaochunguza magazeti, wamewachunguza wanafalsafa, vitabu na makala ya mambo mbalimbali, lakini hata hivyo hawawezi kupata jibu

lolote. Lakini hili hapa linakuja, asubuhi ya leo, katika Biblia. “Asubuhi inakuja, na usiku waja pia.” Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utambariki kila mtu hapa, walioinua mikono yao. Na Wewe unajua kilicho nyuma ya huo mkono ulioinuliwa. Tena, Bwana, ninaamini ya kwamba pale pale walipoketi sasa, kwamba Mungu aliye kila mahali anaweza kuwagawia urithi wao wa Roho wanayemtafuta kwenye saa hii. Mpe kila mmoja, Bwana. Kwa ajili ya Neno Lako na shauku yao, na ahadi Yako ya Kiungo isiyoweza kushindwa, jalia wapokee kile wanachoinulia mikono yao, ninapotoa sala hii kwa niaba yao. Katika Jina la Bwana Yesu, jalia wakipokee. Amina.

Mungu awe pamoja nanyi.

¹²⁵ Sasa tuna muda kidogo tu kwa ajili ya . . . Sasa tutawaombea wagonjwa. Nina furaha sana kujua kwamba kuna tumaini kwa ajili ya wagonjwa. “Mimi ndimi Bwana Yule akusameheaye maovu yako yote, Yule akuponyaye magonjwa yako yote.”

¹²⁶ Na mimi, kiajabu tu jinsi ilivyo, niliongozwa muda mfupi uliopita, kwa maskini mama fulani aliyelala kwenye hii machela. Na yeye ni mwa—mwathiriwa wa ugonjwa wa Limfu. Nami naamini anayeketi hapa pamoja naye ni mama yake. Nina uhakika kabisa. Naam, hiyo ni kweli, kwamba mama huyu alikuwa akiniambia kuhusu mtoto wake, nami nilikuwa nikijaribu kumtia moyo.

¹²⁷ Na wito tu, pia, baada ya ujumbe huu. Ninahisi kwamba wokovu ndio jambo la kwanza. Uponyaji ni wa pili. Uponyaji unaweza kudumu hadi mwisho wa maisha yako, miaka mingi. Unaweza kukupa furaha na shangwe wakati ukiwa hapa duniani, lakini utakoma pamoja na ninii yako. . . hapo utakapokufa. Lakini nafsi iliyookolewa, ina Uzima wa Milele. Haiwezi kuangamia, wala hakuna kitu kinachoweza kuiondoa kwako. Imeingia katika Vitabu vya Mungu, ipate kufufuliwa katika siku za mwisho. Jambo kuu ni kile kitu cha kwanza, “Kwanza, Ufalme wa Mungu na haki Yake, vitu vingine vitaongezewa.”

¹²⁸ Ningependa tu kutoa ushuhuda mmoja wa uponyaji wa ugonjwa huu mbaya sana ambao maskini mwanamke huyu anaangua. Na siku moja kulikuwa na . . . Huenda wapo asubuhi ya leo. Sipo hapa mara nyingi sana kujua nani ni nani. Wengi wenu siwajui. Lakini kulikuwako na msichana mdogo hapa katika shule yetu ya upili. Naye alikuwa anaangua ugonjwa huu wa Limfu, naye akapelekwa kwa daktari, kwa sababu ya uvimbe huu mkubwa uliomtokea. Nao wakachukua kipande cha huo uvimbe na kukituma kwingine, wapate kujua kilikuwa ni kitu gani. Nacho kikarudishwa, “Ugonjwa wa Limfu usiotibika.”

¹²⁹ Naye huyo mama hakutaka mtoto ajue shida yake ni nini. Nao madaktari wakamshauri huyo mama amruhusu tu aendelee na shule, kwa sababu alikuwa na siku kadhaa tu za kuishi.

Hatimaye huvuja ikaingia moyoni. Nao ugonjwa wa Limfu ni kansa, tunajua hilo, katika umbo fulani. Basi wakamrudisha hu—huyo msichana mdogo shuleni, apate kufa.

¹³⁰ Mama akaingia wazimu. Naye akanipigia simu, na kusema, “Nataka kumleta. Lakini ninasikia, Ndugu Branham, ya kwamba katika mistari yako ya maombi, mara nyingi, unataja magonjwa wakati ukiwa na uvuvio wa Roho.” Akasema, “Je, ungekuwa na fadhili sana, ikiwa Roho Mtakatifu atafunua jambo lolote kuhusu huyo mtoto, na usiliseme?”

¹³¹ “Vema,” nikasema, “Sidhani angeufunua, kama hakutaka ujulikane.” Nikasema, “Angalau sidhanii hivyo. Na kwenye maskani yangu mwenyewe hapa, ni kwa nadra ninakuwa na mikutano ya aina hiyo.” Nikasema, “Ninawaomba tu wagonjwa.”

¹³² Ndipo yule msichana akaingia mstarini. Nami nikamuuliza mama yake, “Je, wewe ni Mkristo?”

Akasema, “Hapana.”

Nikasema, “Je, huyo msichana ni Mkristo?”

“La.”

¹³³ Nikasema, “Hiyo ni njia mbaya ya kuondoka ulimwenguni.” Nami nikasema, “Hutamwona tena, kama akienda katika hali hiyo.”

¹³⁴ Kwa hiyo wakati yule msichana mdogo alipoingia chumbani asubuhi hiyo... Naye akapitia papa hapa mahali ambapo yule msichana mdogo aliombewa; basi msichana huyu ataombewa, katika dakika chache. Nilimuuliza. Nilimjua. Nami nikasema, “Je, wewe ndiye yule msichana mdogo kutoka shule ya upili hapa?”

Akasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Je, unaufahamu ugonjwa wako?”

¹³⁵ Akasema, “Madaktari wananiambia kwamba wanafikiri nitakuwa mzima.”

¹³⁶ “Vema,” nikasema, “vipi kama hutakuwa mzima? Je, wewe ni Mkristo?”

Akasema, “La, bwana. Hasha.”

Nikasema, “Je, ungependa kuwa Mkristo?”

Akasema, “Ndiyo.”

¹³⁷ Nami nikasema, “Je, utampa Kristo moyo wako?” Naye akasema angempa. Naye mama yake akakimbia na kusema angempa pia. Ambapo, niliwabatiza wote wawili papa hapa kwenye dimbwi. Nikamwomba maskini msichana huyo.

¹³⁸ Basi wakati ukaendelea. Ndipo hatimaye huyo msichana akaanza kupata nafuu, baada ya siku chache, huku hajui shida yake. Ndipo baada ya muda kidogo, wakamrudisha akafanyiwe

uchunguzi, nao wasingeweza kupata dalili yake, hata kidogo. Kuna . . .

¹³⁹ Sipendi kuongea mambo ya kuwasifia watu, lakini napenda kuwa mkweli kuhusu watu. Kuna mtu humu mjini, ambaye anajulikana sana, na ni ndugu Mkristo mzuri, la sivyo hangekuwa shemasi wa kanisa hili. . . Ninamaanisha, mdhamini wa kanisa. Naye yuko sasa. Naye alijichukulia jukumu la kufuatilia mambo ya msichana huyo. Ilikuwa miaka kadhaa baadaye, miaka miwili au mitatu baadaye, huyo msichana mdogo alikuwa amemaliza shule na alikuwa akiambatana na mvulana fulani.

¹⁴⁰ Nami nikakutana naye mtaani siku moja, naye alikuwa na furaha sana, naye akashuhudia juu ya utukufu na uweza wa Yesu Kristo, wakiisha kumwambia ilikuwa nini. Huyo msichana ameolewa. Ana watoto. Naye anaishi kwa furaha.

¹⁴¹ Naye baba yake huja kwenye biashara ya mtu huyu, kunyolewa nywele zake. Naye Bw. Egan hapa, ambaye ame—amekifuatilia hicho kisa muda huu wote. Naye huyo msichana ni mzima na mwenye afya. Na hiyo imekuwa muda gani, Ndugu Egan? Miaka kadhaa iliyopita, sivyo? [Ndugu Egan anasema, “Miaka minne, mitano, sita iliyopita.”—Mh.] Naye anaishi leo, kwa ushuhuda ya kwamba Mungu huponya ugonjwa wa Limfu.

¹⁴² Loo, ni vizuri sana kujua, kwamba katika saa za dhiki, kwamba tuna kimbilio. Kimbilio hilo ni Kristo.

¹⁴³ Nataka kutoa taarifa kwa . . . kwa wengine wenu, jambo fulani dogo mkutanoni, ambalo limetukia hivi punde. Bwana alikuwa mwema sana katika kujibu maombi yenu nyote, nilipoenda Magharibi kwa ajili ya mkutano sasa hivi, majuma machache yaliyopita, majuma mawili. Basi tulipokuwa huko Tulsa, kwenye mkutano mkuu, nilipaswa . . . sikuwa nihubiri, kwa sababu . . . Nilipaswa kufanya mkutano huko. Lakini wahudumu walikuwa na miamsho mingine ikiendelea, kwa hiyo nisingeweza kufanya mkutano huo wakati huo. Lakini nikapitia huko, kumchukua Ndugu Arganbright, kumpeleka California; mimi na mke wangu, na mtoto Joseph.

¹⁴⁴ Basi usiku huo, tulipoingia tumechelewa, nilisikia ya kwamba Oral Roberts na Tommy Osborn walipaswa kuhubiri usiku huo. Kwa hiyo Ndugu Arganbright akanitafuta kwa simu kwenye hoteli mpaka akapata mahali tulipokuwa, na kusema, “Shukeni mje mkutanoni.” Kwa hiyo akaja huko, yeye na Ndugu Sonmore, Wafanyabiashara Wakristo, kiongozi wa tawi huko Minneapolis. Wao—wakaja kunichukua.

¹⁴⁵ Nami nikaingia, nao tayari walikuwa wakila chakula cha jioni, katika—katika bwalo la Mayo, mahali pazuri sana. Mamilionea wameketi mle ndani. Na basi mnajua jinsi ningejisikia kuingia mahali kama hapo. Hata sikujua jinsi

ya kutumia visu na uma walizokuwa nazo mezani. Lakini nikaingia.

¹⁴⁶ Na wakati nikiingia, Oral Roberts alikuwa akihubiri. Naye alikuwa akihubiri juu ya maisha tele, maridhawa, na kuwaambia Wafanyabiashara Wakristo, kwamba, “Yesu aliwakamata wale samaki, akawatia kwenye nyavu, na walikuwa na zaidi ya wale wangeweza—wangeweza kutumia.” Na Ndugu Roberts huongea kwa nguvu, kama mjuavyo. Naye akasema, “Kuna wengi kwa ajili ya kila mtu.” Kisha akasema, “Sasa, ninajenga he—hekalu hapa, pengine itagharimu mamilioni ya dola.” Akasema, “Imejengwa kwa marmar nyeupe.” Naye akasema, “Nilifika karibu nusu kwenda juu, ndipo nikaishiwa na pesa.” Kisha kasema, “Ndipo nikavuka barabara siku moja, kuiangalia, naye ibilisi akasema, ‘Unajua nini? Watu watapitia hapa na kusema, ‘Hivyo ndivyo Oral Roberts alivyofanya.’”

¹⁴⁷ Akasema, “Ndipo nikamwambia ibilisi, ‘Lakini watalazimika kusema, “Oral Roberts alijaribu.”’” Hilo ni zuri. Kisha akasema, “Ndipo likawekwa moyoni mwa mkurugenzi wa benki, hapa mjini, ambaye alinikopesha nyingi zaidi, karibu, dola milioni mbili kutoka kwenye benki, kulimalizia jengo hilo.” Benki hazifanyi hivyo. Mnajua hilo.

¹⁴⁸ Naye akasema, “Huyo mfanyabiashara fulani, mkurugenzi wa benki, yuko hapa sasa ameketi.” Akasema, “Sitaki kulitaja jina lake, kwa sababu yeye si wa full Gospel hasa. Lakini,” kasema, “yuko hapa.” Kisha kasema, “Si—sidhani hata anadai kuwa Mkristo. Lakini,” kasema, “kitu fulani kiliuongoza moyo wake, akanipa hizo pesa.” Kasema, “Ikiwa anataka kusimama,” kasema, “anaweza, lakini sitamwaibisha huyo mtu.”

¹⁴⁹ Huyo mtu akasimama, akasema, “Sioni haya, Bw. Roberts,” kisha akaketi chini.

¹⁵⁰ Ndipo nikaingia, nami nilikuwa nimeketi chini. Ndipo Ndugu Roberts, mara alipomaliza, akaja na kupeana mikono nami, na kunikumbatia kwa mikono yake. Na dakika chache tu, basi, bila shaka, watu wengi wakakaribia, mwajua, wakizungunza tulipokuwa tungali tunakula, na wakiwa na shauku ya mikutano na kadhalika, na wahudumu.

¹⁵¹ Ndipo basi Demos Shakarian akasimama. Yeye ndiye rais wa tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel. Naye akasimama na kusema, “Mnajua, ninajisikia tu kuongozwa kwamba Ndugu Branham anapaswa kutuhubiria, usiku wa leo, ujumbe wa mwisho.”

¹⁵² Vema, sikujua la kusema. Naye akaanza kusema juu ya watu waliokuwa wameketi humu ndani, kasema, “Huyu hapa *Fulani-wa-fulani*. Nimekutana naye leo.” Walikuwa wakiniambia kuwa wanamiliki bloku hizi zote tatu ama nne za Maili ya Mwujiza. Mamilionea na matajiri wa ng’ombe, na kadhalika, basi ningeweza kusema nini katika mkutano kama huo?

¹⁵³ Lakini, mwajua, daima ni bora kutii. Kwa hiyo nikasimama kuongea vizuri sana nilivyoweza. Basi mwisho wa ibada... Ni kukiuka utaratibu kabisa kutoa wito wa madhabahu mahali kama hapo. Lakini, mnajua, nimefanya wito wa madhabahuni kwenye ibada za mazishi. Kwa hivyo nikawazia, “Hii hapa nafasi nzuri.” Nami ni—nikatoa wito wa madhabahuni. Ndipo hao matajiri wote wanaume kwa wanawake wakamjia Bwana Yesu, na kutoa mioyo yao kwa Bwana.

¹⁵⁴ Nilishangazwa na milionea mmoja, mke wa milionea aliyevaa kofia ndogo, yenye manyoya maridadi chini upande mmoja, pengine ilimgharimu dola mia moja. Huku machozi yakitiririka mashavuni mwake. Akanishika mkono, akasema, “Ndugu Branham, moyo wangu umeguswa.” Akasema, “Nilidhani nilikuwa Mkristo, mpaka sasa.” Akasema, “Nataka kumtumikia Bwana.”

Nami nikasema, “Asante.”

¹⁵⁵ Halafu katika dakika chache, Kitu fulani kikaniambia, “Waombee wagonjwa sasa.”

¹⁵⁶ Nikawazia, “La, hapana. Siwezi kufanya hivyo. Tayari nimekatiza ninii...bwalo hili kubwa. Kwa hivyo nikiombea wagonjwa, watafikiri mimi ni mlokole kweli.” Kwa hivyo nikawazia, “Hakika Bwana asingekuwa ananiambia hivyo. Labda nimechangamka tu kwa sababu ya maongofu haya, kwa hivyo nitaenda niketi chini.”

¹⁵⁷ Nami nikashuka chini kupitia kwenye meza ya spika, hata mwisho kabisa, nikaketi pamoja na Ndugu Jack Moore, aliyekuwa ameketi pale, akizungumza. Nami nikairudisha ibada kwa rais, Bw. Shakarian.

¹⁵⁸ Basi wakati a—aliposimama, akasema, “Mnajua nini?” Loo, hapana budi Mungu alimgusa begani. Akasema, “Ninajisikia kuongozwa kumwita Ndugu Branham arudi na kuwaombea wagonjwa.”

Nikawazia, “Loo, sawa kabisa.”

¹⁵⁹ Nami nikasimama na kuwaambia. Basi nikasema, “Nilihisi hivyo. Nami naomba Mungu anisamehe. Lakini ni bora mtu fulani anapoguswa, pia, mwajua, inatufahamisha kabisa ni matendo ya Roho.”

¹⁶⁰ Kwa hiyo nikasema, “Sasa, uponyaji wa Kiungu sio kugusa nguzo ya mizimu. Si kitu tu cha kuwazia. Ni Mungu yeye yule aliyewaokoa watu hawa wote hapa muda mfupi uliopita. Yeye ni Mungu yule yule anayewaponya watu wote waliopo hapa, kwa imani rahisi tu kumwamini Yeye.” Nikasema, “Je, mnaamini hivyo?”

¹⁶¹ Na sasa tuiendee ile siri, kwa kanisa langu. Kama mjuavyo, huduma yangu inabadilika, na, loo, ni badiliko tukufu jinsi gani! Loo! Ninyi nyote mnakumbuka Maneno ambayo yamekuwa

yakivuma. Na kila yanapotokea, jambo fulani linatukia, ninapoanza kuzungumzia hilo, linakuja—linanijia, “Uambie mlima huu.” Kwa nini imekuwa hivyo? Imekuwa ni imani. Chochote ni kwa imani. Imani sio kitu unachochochea. Imani ni kitu ulicho nacho.

¹⁶² Nami nikawazia, “Kama... Daima nimeionea haya imani yangu, kwa watu, kadiri ambavyo Bwana amekuwa mwema.”

¹⁶³ Ameonyesha mambo, amewaambia maono. Kila kitu kimekuwa kikamilifu. Ninyi watu mnajua hilo. Si mtu binafsi. Si mwanadamu. Ni Mungu anayefanya hivyo.

Nayo picha hii *hapa*, jinsi ilivyoenea ulimwenguni!

Zile zilizoko Ujerumani!

¹⁶⁴ Na *hapa* majuma machache yaliyopita, labda wageni *hapa* hawakuwahi kuiona, walipiga nyingine. Ninayo nyumbani. Ni sura ya Bwana Yesu akisimama papo hapo nyuma ya pale nilipokuwa nimesimama. Nayo mikono Yake imenyoshwa, na ndimi za Moto zikiruka kutoka mkononi Mwake, nilipokuwa nikina juu ya somo hilo, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini.” Nasi tunayo. Iko katika rangi za Tekno... Kodakromu. Nao wanayo nyumbani sasa. Na wanatengeneza... Imechunguzwa sasa na sayansi, na kadhalika, na maabara. Itatokea hivi karibuni sana, nyingine, ambayo inazifanya takriban sita sasa katika sehemu mbalimbali, ambazo zimepigwa.

¹⁶⁵ Hii ndiyo bora zaidi ya zote, haijapata kuonekana. Hizo hapo ndevu Za—Zake, uso Wake, sura ya umbo Lake, mikono Yake ikining’inia. Nami nilikuwa nimesimama moja kwa moja *hivi*, na ambapo Yeye ameweka mikono Yake, hata huwezi kuona mahali pangu, namna hiyo; kichwa changu, kisha miguu yangu chini sakafuni, kichwa na miguu tu, ndiyo yote iliyosalia. Mnaona? Na Yeye—na Yeye amesimama akiwa amenyoosha mikono Yake *hivi*. Nami nimeweka mikono yangu namna *hii*, nikihubiri, nikisema, “Ukiuambia mlima huu.” Na yapata wakati huo, jambo fulani likatukia. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Nao wakapiga picha Yake namna hiyo. Nayo Hiyo hapo, nyuma, yote katika rangi. Na ninii kubwa, jinsi Mungu anavyopanga, kikapu kikubwa cha yungiyungi ya kala kimewekwa karibu.

¹⁶⁶ Yeye ni Yungiyungi la Bondeni. Nawe unapata wapi kasumba? Kutoka kwa yungiyungi. Hiyo ni kweli. Je, Mungu ana Kasumba gani? Amani. Kasumba hukufanya usahau yote kuhusu shida zako. Wavutao kasumba, hivyo ndivyo wanavyojiua kwa hiyo kasumba. Mungu ana Kasumba. Amina. Yeye hupunguza kila maumivu, huponya magonjwa yote, huondoa kila hofu. Maadamu tunapumua ndani ya Kasumba Yake, tuna amani.

¹⁶⁷ Nacho hicho kikapu kikubwa cha yungiyungi kimewekwa papo hapo mbele, mahali nilipokuwa nikizungumzia, jukwaani.

168 Nami nikawaombea wagonjwa, huko Tulsa, nami nikashuka tu na kutoka. Na yapata dakika kumi baadaye. . .

169 Nisingependa kulitaja jina la huyo mwinjilisti. Lakini mwanamke aliyekuwa na yabisi kavu ya uti wa mgongo, ambaye alimfanyia kazi mwinjilisti huyu, alikuwa mwandishi wa hatimkato. Naye ilimbidi kupiga chapa namna *hii*, maana mikono na mabega yake yalikuwa yamefungwa. Alipiga chapa namna *hiyo*. Naye huyu—huyu mwinjilisti mkuu na mashuhuri huko Tulsa, alimwajiri katika ajira yake, kumpa kazi.

170 Basi akaanza kushuka ukumbini. Na kwa ghafla mikono yake ikanyoka, akaanza kuruka-ruka na kupiga mayowe, mpaka akavutia usikivu wa kila mtu kule juu. Naye mwanamke huyo mpendwa akipiga magoti, na kuinua mikono yake na kupiga makofi namna *hiyo*. [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] Utukufu wa Mungu, kwa sababu Mungu alikuwa amemweka huru, muda mfupi tu baada ya maombi.

171 Nami nikanyemelea ndani, kusikiliza nione kile alichokuwa akisema. Akasema, “Nilikuwa tu nikishuka ukumbini.”

Nami nikasema, “Vema, Mungu ashukuriwe.”

172 Nami nikageuka, nikaanza kutembea upande huo mwingine. Nami nikasikia, huko chini kabisa, nikaona wenye dhambi wote wakikimbia pamoja, kuona kuna nini. Na huyu hapa mtu akiongea, Ndugu Gardner, mtu yule yule aliyenipa suti hii.

173 Wengi wenu mnamjua Ndugu Gardner. Ndugu Gardner, huko Binghamton, New York, yule bingwa mashuhuri muuza Oldsmobile kwa miaka mitatu iliyopita, aliuza magari mengi sana ya Oldsmobile kuliko mtu mwingine yeyote nchini Marekani. Naye anaruka kwa ndege ya kibinafsi. Na kidogo zaidi ya mwaka mmoja uliopita . . . Jina lake ni George Gardner. Naye. . .

174 Rubani wake, yeye mwenyewe, alikuwa akijiendesha, naye akaanguka, kwa ndege. Akapasuka magoti yake, tindi za miguu yake. Nayo miguu na nyayo zake zilikuwa zimeshupaa, naye alitembea *hivi*, rubani wake.

175 Naye alikuwepo wakati hayo maombi yalipofanywa, naye alikuwa amejitoa nje ya ukumbi ambako ile dhifa ilifanyiwa. Na walikuwa wamemwandalia chumba hapo karibu, pia, asiye akasumbuka akitembea huku na huku. Basi ushuhuda wake ulikuwa hivi. Alikuwa ameenda chumbani mwake na kuketi chini; hata hakuwa Mkristo. Naye akasema, “Kwa namna fulani, ninamwamini maskini jamaa huyo mwenye upara aliyehubiri kule juu usiku wa leo.” Naye akasema alianza kuona vidole vyake vya miguu vikianza kutikisika. Ndipo akaruka kwa miguu yake, mzima kabisa.

¹⁷⁶ Akisimama huko nje, akimtukuza Mungu, amesimama, akiinua miguu yake juu-chini namna *hiyo*, na kando ya miguu yake na kila kitu, akishuhudia tu kwa utukufu wa Mungu.

¹⁷⁷ Mara nyingine tena, kabla hatujawaombea wagonjwa. Nilikuwa nikikaa pamoja na Ndugu Arganbright. Naye rafiki yangu mwema, Leo na Gene, anajua kupiga simu ni nini. Simu zikilia, naye Ndugu Arganbright angejibu. Na, unajua, huwezi kuwa kila mahali. Lakini, ikawa, kwamba nilichukua simu.

¹⁷⁸ Ninaamini kila kitu hufanya kazi kwa njia iliyowekwa na Mungu. Hivi hamwamini? Ninaamini hiyo ndiyo sababu huyu msichana yuko hapa. Ninaamini hiyo ndiyo sababu nyote mko hapa. Ninaamini hiyo ndiyo sababu mimi niko hapa, kwamba tumekutana pamoja kwa utukufu wa Mungu, kwa sababu fulani. Kwa nini tukaja kupitia maeneo yaliyojaa barafu, tupate kuwa hapa asubuhi ya leo?

¹⁷⁹ Kwa hiyo nikachukua simu, maana Ndugu Arganbright hakuwamo chumbani. Nayo ikasema, “Ningependa kuzungumza na Ndugu Branham.”

Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

¹⁸⁰ Alikuwa Mhispania. Akasema, “Bwana, najua karibu si busara, kwangu kuuliza swali nitakalouliza.” Akasema, “Ninaweza kuwazia jinsi watu wanavyovuta, na kadhalika. Lakini,” kasema, “Mimi ni mmishenari huko Meksiko.” Kisha kasema, “Nyuma huku, ninaishi hapa La Crescenta. Nami nimesikia hivi punde, saa chache zilizopita, ya kwamba ulikuwa mjini.” Kisha kasema, “Nilimrudisha mtoto wangu, kujaribu kukuletea wewe au Ndugu Roberts, au baadhi ya ndugu wanaowaombea wagonjwa.” Naye akasema, “Kwa kuwa ni mtoto wangu mchanga, imani yangu, nadhani, imekuwa tu dhaifu kidogo.” Akasema, “Mtoto wangu bado hajafikisha miezi minne na yuafa kwa kansa.”

Ndipo Kitu fulani kikaniambia, “Mwendee huyo mtoto.”

¹⁸¹ “Vema,” nikasema, “bwana, nitamchukua Ndugu Arganbright, nawe umwambie mahali mtoto huyo alipo, nitakutana nawe.” Kwa hiyo anapata... Ninamchukua Ndugu Arganbright, naye anamwambia.

¹⁸² Basi tukaingia kwenye gari na kuelekea huko. Nami nikakutana na maskini mke wake. Naye akiwa ni Mmeksiko, ingawa hakufanana nao. Alikuwa ngozi nyeupe, mweupe, lakini alikuwa Mmeksiko. Ambao, Wameksiko, mara nyingi, ni wa kimanjano, kwa sababu wanakuja kati ya Wahispania na Wahindi. Na kuna baadhi ya hao Wahindi wenye rangi ya manjano tu, weupe kama theluji. Halafu mkewe alikuwa Mfini, manjano kabisa, mwanamke wa kuvutia sana.

¹⁸³ Basi nikaenda hospitalini pamoja naye, kumwona mtoto wake mchanga. Nilipoingia chumbani, walikuwa wamemweka

papo hapo karibu na makao makuu ya wauguzi. Kwa maana, huyo mtoto mchanga, hajafika bado umri wa miezi minne, naye alizaliwa na uvimbe wa kufisha kwenye taya, ambao ulivimba yapata umbali *huo* kutoka usoni mwake, namna *hiyo*, umetokeza tu namna hiyo. Nao madaktari walikuwa wamejaribu kumfanyia upasuaji. Na makovu makubwa mno yenye kilindi yalikuwa yamekatwa kuzunguka koo lake dogo, pande zote. Haikuizua; ila iliitapakaza kwenye ulimi wake. Na hizo taya ndogo zimening'inia namna *hiyo*, na hayo makovu makubwa yenye kilindi. Nao maskini ulimi wake mdogo . . . Kinywa kidogo si kikubwa kuliko *hivi*. Nao ulimi wake, labda ukubwa *huo*, umevimba, ulikuwa umetokeza nje yapata umbali *huo*, na ukawa mweusi. Nao ukaziba pumzi kutoka puani kushuka chini, ulipovimba kwenye paa la kinywa chake. Na bila shaka, ulikataza pumzi yake, kutoka *hapa*. Ilibidi watoboe tundu kooni mwake. Naye alikuwa na kijifilimbi cha ninii ndogo . . . kama kijibati cha duara kwenye koo lake. Nayo maskini mikono yake ilikuwa katika magango, namna *hii*, asiye akainyosha akaking'oa kijifilimbi hicho; angesongwa roho. Nayo hiyo kansa, ikinyonya, naye nesi ilimbidi kusimama hapo ameshika kitu cha kunyonya mtoko wa hiyo kansa kutoka kwenye hicho kijifilimbi, la sivyo ungemsonga roho hadi afe.

¹⁸⁴ Ndipo huyo baba akaenda kando ya kitanda, akasema, “Ricky, mvulana mdogo wa baba!” Akasema, “Baba amemleta Ndugu Branham akuombe, Ricky.”

¹⁸⁵ Aliposema, “Mvulana mdogo wa baba,” roho yangu ikaniacha tu. Nisingeweza kuvumilia zaidi. Ilinibidi nishikilie tu kando ya kitanda. “Mvulana mdogo wa baba.” Naye maskini jamaa huyo, bado angali mchanga jinsi alivyokuwa, alijua alikuwa baba yake. Ndipo akaanza kukoroma namna hiyo, na mikono yake midogo namna hiyo. Naye akijaribu kumpapasa maskini huyo jamaa mdogo kichwani. Maskini mtoto mchanga, aliyezaliwa katika hali hiyo. Kamwe nisingeweza kuzungumza. Nilininii tu . . . Mwajua, unazidiwa sana, hata huwezi kusema chochote.

¹⁸⁶ Nikaangalia chini, nikaona hiyo mikono midogo sana huko chini ya magango hayo makubwa. [Ndugu Branham anatoa sauti ya kukoroma—Mh.] Na kufanya sauti ya kukoroma. Ndipo nikawazia, “Je, si ni masikitiko hayo!”

¹⁸⁷ Ndipo nikishajirudia kwa namna fulani, vya kutosha kuwazia jambo fulani, niliwazia, “Yesu, unamaanisha kwamba unapata furaha kwa kuona hayo? Siwezi kuamini. Kamwe siwezi kuamini ya kwamba unapata utukufu kwa kuteseka kwa mtoto huyo mchanga namna hiyo. Kamwe haiwezekani. Kama inanifanya mimi, mwenye dhambi, kujisikia kama ninavyojisikia kwa mtoto huyo, ingekuwa Kwako, chemichemi ya rehema zote? Je, inapaswa kukufanyaje?” Wala sikuwa nimesema neno lolote bado.

¹⁸⁸ Alikuwa akijaribu kucheza naye, kumtuliza. Na maskini mwili wake umevikwa nepi ndogo, yapata tu...Huo mwili mdogo, na kadhalika, sio zaidi ya ukubwa *huo*. Nacho kichwa chake kilikuwa ndiyo sehemu kubwa zaidi, taya yake imevimba sana. Nao walifunika kichwa chake kwa kitu fulani, maskini kichwa chake kisije kikapasuka. Mnajua, kitambaa; taya zake zilikuwa zimevimba sana, zimetokeza namna *hiyo*, kisije kikapasuka. Naye nesi alikuwa amesimama hapo.

¹⁸⁹ Ndipo nikamtazama huyo jamaa mdogo, nikawazia, “Bwana, ungefanya nini Wewe kama ungalikuwa umesimama hapa?”

¹⁹⁰ Sasa, ninatambua ya kwamba niko mimbarani. Na ninatambua kwamba Mungu yupo. Lakini ilionekana kwangu kwamba kitu Fulani kilinena nafsini mwangu, na kusema, “Nangojea nione utakalofanya kulihusu. Nililipa Kanisa mamlaka Yangu.” Hapo unarudi tena kwenye, “Ukiuambia mlima huu.” “Nililipa Kanisa mamlaka Yangu, nami ninangojea nione kile utakachofanya.”

¹⁹¹ Nashangaa kama huo ndio mtazamo Wake kwetu kila wakati, kwamba Yeye anangojea aone kile tutakachofanya. Vipi kuhusu ishara za wakati ambazo tumekuwa tukihubiri juu yake? Angefanya nini? Anangojea aone tutakachofanya.

¹⁹² Vema, nikaweka mkono wake wa kitoto mkononi mwangu, kwenye vidole vyangu tu, namna *hiyo*. Ulikuwa mdogo sana. Nami nikasema, “Bwana, yasikie maombi ya mtumishi Wako. Na kwa imani, kwamba ninaamini ya kwamba ndivyo ulivyo Wewe, ninaweka kati ya pepo huyu wa kansa na maisha ya huyu mtoto, Damu ya Yesu Kristo. Kati ya muuaji na huyu mtoto mchanga, Damu, kwa imani naiweka *hiyo*.” Wala nisingeweza kusema kingine chochote.

¹⁹³ Niligeuka tu nikaanza kutoka nje. Baba yake akanifuata. Akasema, “Ndugu Branham, Bwana anaweka juu ya moyo wangu kukupa zaka kidogo.”

¹⁹⁴ “Loo,” nikasema, “ndugu, usifikirie hilo. Hapana.” Nikasema, “Sihitaji pesa, ndugu.”

¹⁹⁵ Akasema, “Lakini niliweka akiba zaka kidogo.” Loo, pesa kidogo, ninasahau sasa ni ngapi hasa, ninaamini yapata dola hamsini. Akasema, “Bwana aliliweka moyoni mwangu nikupe wewe.”

¹⁹⁶ Nikasema, “Hebu nikwambie. Nitazipokea, kisha uzirudishe na kumpa maskini Ricky pale, kwenye—kwenye bili yake ya hospitali. Maana, wewe ni mhubiri. Najua jinsi ilivyo, kile pesa inachomaanisha. Nawe, mmishenari, nami najua kwamba inahitaji pesa. Nawe una familia, na bili hizi zote za daktari. Zirudishe moja kwa moja kwenye bili ya mtoto Ricky.”

197 Akasema, “Sitaki kufanya hivyo, Ndugu Branham. Si za kuwalipa madaktari. Ni za kuwalipa wahudumu.”

198 Nami nikasema, “Naam, lakini ninazirudisha kwako.” Nami nikazikataa.

199 Basi nikaenda nyumbani, na baada ya saa chache, taya hizo zikashuka, nao ulimi wake ukarudi mahali pake pa kawaida. Mungu akamponya maskini jamaa huyo. Walikuwa wakiondoa kile kijifilimbi asubuhi niliyoondoka, kutoka kooni mwake.

200 Iliishtusha sana Pwani yote ya Magharibi. Daktari maarufu akamtuma mwanawe, pamoja na mjukuu wake. Nao wakafunga njia, huko mbali sana, zaidi ya maili arobaini ama hamsini, huko Pasadena, nao wakafunga njia niliyopaswa kupitia, kumwomba mtoto huyo ambaye alikuwa na mshtuko wa mishipa kwenye ubongo. Walikuwa wamemdunga sindano ya penisilini, na kusababisha kushikwa na kansa kutokana na athari za sindano ya penisilini nyongani mwake. Nami nina hakika Bwana alimponya.

201 Kabla tu ya kuondoka nyumbani, simu ikalia, ikaendelea kulia. Ndugu Arganbright, nilimsikia akibishana na mtu fulani, akasema, “Hapana, nisingefanya hivyo.”

202 Wakati tu nilipokuwa nikiingia kwenye gari, ga—gari dogo la abiria na mizigo likaingia. Alikuwa ni nani ila maskini ndugu yangu Mmekisiko na mkewe! Wote wawili wakilia tu na kumsifu Mungu. Wakasema, “Ndugu Branham, nilikuletea zaka hizi.”

203 “Loo,” nikasema, “ndugu, siwezi kupokea hizo.” Nikasema, “Kamwe nisingeweza kufanya hivyo.”

Akasema, “Lakini nimezileta kwako.”

Kasema, nikasema, “Nilikwambia uziweke kwenye bili ya Ricky.”

204 Akasema, “Asubuhi ya leo, nilipoenda kumpa daktari zaka hizi, ziwekwe kwenye bili ya Ricky, daktari alisema, ‘Sikudai chochote.’ Akasema, ‘Sikuhusika nalo kwa chochote.’ Akasema, ‘Hilo ni tukio la ajabu mno.’ Akasema, ‘Mimi... Sikudai hata senti moja.’ Kwa hivyo akasema, “Chukua hizi, Ndugu Branham. Bwana aliniambia ulikuwa uzichukue.”

205 Nikawazia, “Loo, siwezi.” Nikasema, “Bwana, sijisikii kufanya hivyo.”

206 Kisha jambo fulani likanijia. Yesu akisimama siku moja, akiwatazama matajiri wakimwaga pesa zao kwa wingi. Loo, walikuwa na nyingi sana, kwa hiyo walikuwa wakitoa kwa wingi. Ndipo maskini mjane mmoja akaja na senti tatu, na ndizo zote alizokuwa nazo. Hiyo ndiyo akiba yote aliyokuwa nayo, naye akaitia ndani. Sasa tungelifanya nini? “Loo, dada, usifanye hivyo. Huh-uh. Unajua, hatuhitaji hiyo. Usitie hiyo ndani. Hiyo ni riziki yako yote.” Lakini Yesu alimwacha tu aendelee na kufanya hivyo, kwa maana, “Ni heri kutoa kuliko kupokea.”

207 Nikachukua hizo zaka chache. Sijui nifanye nini nazo. Nitaziweka mahali fulani, katika kazi fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu, mahali fulani vizuri niwezavyo.

208 Ni kitu gani? Ni Utukufu wa Mungu. Ni Nguvu za Mungu. Vivuli vinaanguka; Kristo anatokea, hiyo ndiyo sababu ishara na maajabu yanaonekana. Ni ile Nuru kuu ya Mwana ikiakisi kutoka kwenye nyota za asubuhi, yenye uponyaji katika mbawa Zake. Na kama ataleta uponyaji kutoka katika uakisi wa Uwepo Wake, atafanya nini atakapokuja Yeye Mwenyewe? Miili hii yetu iharibikayo itabadilishwa na kufanywa kama Mwili Wake Mwenyewe wa utukufu. Itakuwaje atakapokuja? Mpaka atakapokuja, tunashukuru kwa ajili ya Nuru ya Mwana ya Uwepo Wake, kama vile nyota za asubuhi zinavyopanda ngome za Utukufuni, na kukaa pale kushangilia Kuja Kwake katika wakati huu wa giza.

Na tuombe.

209 Ee Bwana, tunakupenda sana hata, Bwana, hatujui ni muda gani... Hatuchoki kushuhudia sifa Zako. Lakini saa imewadia sasa, kuna wagonjwa wanaongojea. Wewe wajua shuhuda hizi. Hizi, nijuavyo mimi, Bwana, ni za kweli kabisa. Za yule rubani aliyesimama huko nje, akionyesha jinsi angeweza kusimama kwa miguu yake, na hali zote ambazo mwili wake ulikuwa nazo; kisha akavuta miguu ya suruali yake na kuonyesha magoti na miguu yake ilivyopasuka kabisa na imejaa makovu, ambapo madaktari walikuwa wamejaribu kurudisha mifupa pamoja. Ulimwona yule mwanamke aliyesimama pale akiwa amejipaka rangi usoni mwake, huku ikioshwa kwa machozi ya shangwe, huku akisimulia juu ya ugonjwa wake wa yabisi kavu ulivyokuwa umeponywa na Nguvu Zako. Na juu ya yule mtoto mchanga mpendwa, na ushuhuda wa baba yake na wale waliokuwepo.

210 Sasa, Bwana, Wewe ni mkuu tu hapa asubuhi ya leo, hapa maskanini, kama vile ulivyo popote ulimwenguni. Nawe umeahidi ya kwamba mahali ambapo tungekutana pamoja, ya kwamba Wewe ungekuwa katikati yetu. Sasa tutawaita wagonjwa ambao umetutumia asubuhi ya leo. Nasi tutawaombea, na tutaomba kwa mioyo yetu yote, maombi ya imani. Naomba uwaokoe wagonjwa na kuwainua. Na kama wametenda dhambi, wasamehe, Baba, tunapoungama makosa yetu sisi kwa sisi, na kuombeana. Na Wewe umesema, "Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."

211 Tunajua habari za mmoja aliye hapa pamoja nasi asubuhi ya leo, mama mdogo tu akiwa na watoto hawa wadogo. Bwana, kulingana na madaktari, yuko karibu na mwisho wa safari yake. Lakini tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utasimama kati yake na adui huyo. Ndipo tunapomtia mafuta na kumwomba, naomba Nguvu Zako ziguse hiyo nafsi yake. Hiyo italeta imani

na ukombozi. Na jalia aende nyumbani na kupata afya, na kutoa sifa, na awe u—uakisi wa Nyota ya Asubuhi, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

²¹² Ndugu Mercier, sasa, tunapowachukua watu hawa kwa miadi, watu wanaokuja. Tutaita tu nambari hii. Nao watawekwa kwenye orodha ya wale watakaombewa.



MLINZI, HABARI GANI ZA USIKU? SWA58-1130

(Watchman, What Of The Night?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 30 Novemba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org